UWAJIBIKAJI

# Udhibiti wa usajili bajaji, pikipiki za umeme ulivyo 'kaa la moto'-2

Gadiosa Lamtey, Mwananchi
mwananchipapers@tz.mwananchi.com

**Dar/Dodoma.** Sehemu hii inaangazia hali ya mamlaka husika kutupiana mpira kuhusu usimamizi wa bajaji na pikipiki za umeme, hususan katika kuhakikisha zinakidhi matakwa ya kisheria ikiwamo usajili, bima, na utambuzi wa namba za vyombo.

Moja ya changamoto ni kwamba bidhaa za pikipiki zinazotumia nishati ya umeme zilikuwa zikiingizwa nchini kama vipuri, kisha kuunganishwa na kuanza kutumika kibiashara bila kufuata taratibu za usajili.

Kiongozi wa Idara ya Sheria katika Idara ya Usalama Barabarani, Kamishna wa Polisi Mussa Manyama, anasema kuendesha gari lisilosajiliwa, iwe la mafuta au umeme, ni kinyume cha sheria na husababisha hatari kubwa za kiusalama.

Anasema, kama ilivyo kwa magari ya kawaida, kuendesha magari yanayotumia umeme bila kusajiliwa ni kosa linalostahili faini kubwa na kukamatwa kwa chombo husika, kwani hukosa bima na kuwaacha madereva, abiria, na watumiaji wengine katika mazingira magumu baada ya ajali.

Hata hivyo, hakutoa takwimu za kina kuhusu waliokamatwa au kuondolewa barabarani tangu tangazo la Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

"Tutaendelea kutekeleza sheria na kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa usajili wa vyombo vya moto vinavyotumia dizeli, petroli au umeme," anasema.

Meneja Usafirishaji Barabarani na Leseni wa Mamlaka ya Usafirishaji Ardhini (Latra), Patel Ngereza, anasema changamoto za usajili wa magari yanayotumia nishati ya umeme bado zipo, ingawa uelewa wa wananchi unaongezeka taratibu.

Anasema kati ya pikipiki zaidi ya 22,000 zilizosajiliwa Latra mwaka 2025, takribani asilimia nane zinatumia umeme. Anaongeza kuwa licha ya jitihada za kuhamasisha usajili mwaka jana, mwitikio wa wadau haukuwa wa kuridhisha.

Ngereza anasema awali bidhaa za pikipiki zinazotumia umeme zilikuwa vinaingizwa nchini kama vipuri kisha huunganishwa na kuanza kutumika kibiashara.

"Hali hiyo ilitulazimu kuitisha vikao vya wadau kujadili umuhimu wa usajili na utoaji wa leseni za kibiashara," anasema, akibainisha pia kuimarishwa kwa ushirikiano kati ya taasisi yake na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika kushughulikia changamoto mbalimbali ikiwemo ubora wa betri na vifaa.

"Pia, tulibadilisha kanuni zetu kuruhusu magari ya umeme kusajiliwa na kupewa leseni za kibiashara," anasema, pasipo kutoa takwimu za utekelezaji, akisema lengo ni kuongeza elimu kwa umma.

### Kauli ya TRA

Mkurugenzi wa Huduma kwa Walipa Kodi na Elimu wa TRA, Richard Kayombo, anasema magari yanayotumia nishati ya umeme yanafuata mfumo wa namba unaotumika kwa magari ya dizeli na petroli, na wamiliki wanapaswa kulipa kodi za uingizaji.

**RIPOTI MAALUMU**

Anasema Jeshi la Polisi kitengo cha usalama barabarani ndilo lenye mamlaka ya kukamata magari yasiyosajiliwa. "Wajibu wetu ni kutoa matangazo ya kuhamasisha usajili, lakini kukamata wanaokiuka sheria ni jukumu la polisi wa usalama barabarani," anasema.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, anasema wamiliki wa bajaji na pikipiki za umeme zisizosajiliwa wanakiuka sheria. Wilaya inashirikiana na Jeshi la Polisi kukamata vyombo hivyo na kuhakikisha vinafuata sheria.

"Tunaendelea kutoa elimu kwa umma na kushirikiana na watoa huduma za usafiri mtandaoni kukuza shughuli rasmi. Wakati wa ukaguzi, hatua za kisheria huchukuliwa, ikiwemo faini," anasema.

### Shirika la haki za abiria

Mkurugenzi wa Shikuhata, Ambakise Mwakifwange, anasema usafiri wa vyombo visivyosajiliwa unadhoofisha usalama, uwajibikaji, na imani ya umma na kwamba bila usajili, ajali haziwezi kufuatiliwa ipasavyo, kesi haziwezi kuendeshwa, na fidia haiwezi kutolewa.

Anaitaka Serikali kufanya ukaguzi maalumu, kutoa elimu kwa madereva na abiria, na kutunga kanuni mahsusi kwa vyombo vya umeme.

### Wasemavyo Tira

Mkurugenzi wa Utekelezaji na Huduma za Uthaminishaji wa Mamlaka ya Huduma za Bima Tanzania (Tira), Alex Rocky, anasema awali kulikuwa na changamoto kutoa bima kwa magari yasiyo na usajili.

Anasema baada ya tangazo la TRA Mei 15, 2025, magari ya umeme yameanza kusajiliwa na kupewa bima.

"Fidia haitolewi kwa magari yasiyo na bima halali. Magari yasiyo na usajili au bima huwaacha wahanga bila haki za kisheria na kuathiri ustawi wa jamii," anasema. Tira inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu usajili na bima, na inahimiza kampuni za bima kubuni bidhaa maalumu kwa magari ya umeme.

### Kauli ya Taema

Tony Mlela, mwanachama wa Tanzania Electric Mobility Association (Taema) anasema kabla ya sheria baadhi ya bajaji na pikipiki za umeme ziliendeshwa bila kusajiliwa. Taratibu mpya zinaendelea kurekebisha dosari, na baadhi ya vyombo tayari vimeshasajiliwa.

Anasema kanuni za Taema zinalenga ukuaji endelevu wa sekta hiyo, zikizingatia uzoefu wa Rwanda, Kenya, Uganda, na Ethiopia.

### Kauli ya wafanyabiashara, wananchi

Uchunguzi wa *Mwananchi* umebaini kuwa idadi kubwa ya bajaji na pikipiki hizo zinazofanya shughuli zake katika miji ya Dar es Salaam na Dodoma zinaendeshwa bila kusajiliwa, bila kuwa na bima, na bila kubandikwa namba za usajili, hali inayokiuka matakwa ya kisheria.

"Ni vigumu kumfuatilia dereva ambaye bajaji au pikipiki yake imehusika katika ajali au uhalifu kwa sababu mara nyingi hukimbia baada ya tukio," anasema mfanyabiashara wa Kariakoo, Mussa Kinabo.

> **"Magari yasiyo na usajili au bima huwaacha wahanga bila haki za kisheria, yanaongeza umaskini na kuathiri ustawi wa jamii. Kila chombo cha moto kinachotembea barabarani kinapaswa kuwa na bima."**
>
> Mkurugenzi wa Utekelezaji na Huduma Tira, Alex Rocky

"Bajaji na pikipiki zisizosajiliwa huongeza ukubwa wa tatizo kwa sababu ya ugumu wa kuwakamata na kuwachukulia hatua, hasa kwa sababu pia ya kukosekana kwa ushahidi wa utambulisho wa chombo kilichohusika na tukio," anaongeza.

Mfanyabiashara wa jijini Dodoma, Happy Silvano, anasema mahitaji ya usafiri yanaongezeka kwa kasi, jambo linalowalazimu baadhi ya wamiliki kuendesha vyombo hivyo bila kusajiliwa.

"Sijawahi kusikia dereva ametozwa faini, jambo linaloonesha changamoto kubwa katika utekelezaji wa sheria za usalama barabarani, licha ya kuwa tunafanya nao kazi kila siku," anasema.

Wananchi wanasema licha ya vyombo hivyo vinavyotumia umeme kuwa nafuu, kuendesha bila usajili kunazidisha hatari ya ajali, uhalifu, na upotevu wa mapato ya Serikali kutokana na kutokusanywa kwa faini na adhabu za usajili.

"Bajaji na pikipiki nyingi hupata ajali na kuwaacha watu wengi na ulemavu wa kudumu, hasa kutokana na ongezeko la ajali na vitendo vya uhalifu katika majiji haya," anasema mkazi wa Dar es Salaam, Simon Lunda.

"Kuongezeka kwa mahitaji ya usafiri wa haraka kunachochea uhalifu na uporaji. Wengine hunyang'anya simu na vitu vya thamani wanapokuwa barabarani, abiria wanaotumia usafiri wa umma na madereva wa magari binafsi hasa vyombo vyao vinapokuwa kwenye foleni," anasema mkazi wa Dodoma, Linda Kisasa, na kuongeza kuwa baada ya kutekeleza uhalifu hutokomea haraka.

Dereva wa daladala jijini Dar es Salaam, Hamisi Doto, anasema gari yake iliwahi kugongwa na bajaji inayotumia umeme na kwamba baada ya kubaini haikusajiliwa na haikupata madhara makubwa, aliamua kuendelea na safari.

"Kama ingekuwa gari au pikipiki iliyosajiliwa, tungezungumza na baadaye ningelipwa fidia," anasema, na kuhoji kiasi cha mapato ambacho Serikali inapoteza kwa kutokusanya faini na adhabu za usajili.

Mfanyabiashara wa eneo la Jamhuri jijini Dodoma, Rita Massawe, anasema bajaji na pikipiki za umeme hazitoi kelele kama zile zinazotumia dizeli na petroli.

"Siku moja nilikaribia kugongwa kwa sababu zilifika kimya kimya mahali nilipokuwa nimesimama," anasema, akiongeza kuwa mara nyingi wanapohusika na ajali au uhalifu hukimbia toka eneo la tukio.



*Itaendelea kesho*

# Treni 5 SGR kubeba mizigo bandarini Dar kwa siku

Na Shakila Mtambo

SERIKALI imetaja mikakati ya kupunguza msongamano wa makasha ndani ya Bandari ya Dar es Salaam ikiwemo kuongeza safari za Treni ya Kisasa (SGR) ya mizigo.

Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa alisema kuanzia Febuari 15, serikali itaongeza treni tano za mizigo kusafirisha makasha kupeleka bandari ya Kwala mkoani Pwani na Ihumwa, Dodoma.

Profesa Mbarawa alieleza hayo jana alipotembelea na kukagua bandari hiyo na kuona msongamano wa makasha uliotokana na kuongezeka kwa ufanisi wa bandari katika kushusha mizigo baada ya uwekezaji wa DP World na kampuni ya Tanzania East Africa Gateway Terminal.

Profesa Mbarawa alisema kwa sasa bandari hiyo inapokea treni moja ya mizigo inayoweza kubeba makasha 200, hivyo ongezeko la treni tano kutasaidia kupunguza msongamano.

"Bandari ya Dar es Salaam kwa siku ilikua inakuja treni moja ambayo ilikua inachukua makontena (makasha) 200 sasa tumekubaliana itakapofika kuanzia Februari 15, tutaongeza treni tano na bado tuna treni nyingine tano tuna treni 10 zinazoweza kutoa huduma, haya yote tunafanya ili bandari yetu iweze kupumua," alisema.

Aidha, Profesa Mbarawa alisema uwekezaji wa bandari pia umeongeza mapato ya bandari kutoka Sh bilioni 700 kwa mwaka mpaka Sh trilioni 2.03 kwa sasa.

Sambamba na kuongeza safari za treni ya mizigo, serikali imesema Kampuni ya East Africa Gateways Terminal inaendelea na ujenzi wa Bandari kavu ya Kurasini itakayosaidia pia kupunguza msongamano katika bandari ya Dar es Salaam.

Ujenzi wa bandari hiyo ya Kurasini umefikia asilimia 90 na unatarajia kukamilika mwishoni mwa Februari huku kipande cha kwanza kitakua na uwezo wa kuhifadhi makasha 150,000.

Profesa Mbarawa alisema uwekezaji wa kampuni hizo binafsi umeongeza idadi ya makasha yanayohudumiwa kutoka 800,000 mwaka 2020 hadi 1,300,000 mwaka 2025 ongezeko la asilimia 50 na matarajio ni kufikia makasha milioni mbili. Naye Kaimu Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Abeid Gallus alisema ufanisi wa wawekezaji umewezesha kupunguza muda wa kushusha mizigo kutoka siku saba mpaka siku tatu huku wastani wa meli kusubiri nangani umepungua hadi siku tano.

Mkuu wa wa Uhusiano na Uratibu wa Shughuli za Kampuni kutoka DP World, Elitunu Mallamia alisema hadi kufikia Januari 2026 kampuni hiyo imehudumia makasha kwa asilimia 68 kulinganisha na kipindi kama hicho 2025 huku kwa Desemba 2025 kampuni hiyo ilihudumia makasha kwa asilimia 94 kulinganisha Desemba 2024 ikionesha kuna ongezeko la makasha yanayohudumiwa na kampuni hiyo.

CamScanner